Nimeshapita miaka ya kupata mimba yaani nimemaliza ugumba. Je bado nahitaji kupimwa njia ya uzazi?

Ndio, hatari ya kupata saratani katika njia ya uzazi huongezeka kwa umri. Kama umeshawahi kufanya mapenzi, hata kama na mme mmoja peke yake, ni muhimu kupimwa baada ya kila miaka miwili hata baada ya kupita ugumba au hata kama umepita miaka ya kupata mimba.

Nimeona damu isiyo ya kawaida

Ukivuja damu namna isiyo ya kawaida au ukitokwa na usaha katika sehemu za siri, muone daktari haraka iwezekanavyo.

Sikumbuki mara ya mwisho nilipopimwa njia ya uzazi

Daktari wako au hospitali wanaweza kuwa na mpangilio wa kukukumbusha wakati wako wa kupimwa ukifika. Kila mkoa una nakala wanapoadika majibu yako baada ya kukupima njia ya uzazi. Wakati wako wa kupimwa au wa matibabu ukipita, utaandikiwa barua ya kukukumbusha. Mwambie daktari kama hutaki taarifa yako kuorodheshwa au hutaki kupokea barua za kukumbushwa.

Je naweza kupimwa njia ya uzazi wapi?

Unaweza kukubaliana na dakitari, mwuguzi au hospitali ya mpango wa uzazi iliyo karibu na unapoishi wakati maalumu wa kwenda kupimwa. Unaweza kuwauliza ili daktari wa kike au muuguzi wa kike awe ndiye atakaye kupima. Kama unataka mtafsiri awepo, sema hivyo unapopanga wakati wa kuja kupimwa. Ni sawa pia kama utaandamana na rafiki au ndugu yako.

Nimesikia kuhusu chanjo mpya inayoweza kuzuia saratani ya njia ya uzazi

Ndio, chanjo ipo inayoweza kuzuia magonjwa ya aina ya HPV ambayo wakati mwingi husababisha saratani katika njia ya uzazi. Chanjo hiyo imeidhinisha Australia kwa wanawake walio na kati ya umri wa miaka 9 mpaka 26.

Chanjo ya HPV ni bure na ipo chini ya Mpango wa Chanjo Kote Nchini.

Ni bora zaidi kama wasichana watachanjwa kabla hawajaanza kufanya mapenzi. Chanjo hii inakusudia kuzuia saratani ya njia ya uzazi katika vizazi vijavyo vya wanawake. Kama una umri wa miaka kati ya 12 na 26 au una binti wa umri wa miaka 12 na 26, shauriana na daktari juu ya kupata chanjo hii.

Ni muhimu pia kupimwa mara kwa mara maana chanjo itazuia baadhi ya aina ya HPV inayosababisha saratani ya njia ya uzazi.

Kupimwa mara kwa mara ni muhimu kwa maana chanjo ya HPV haizuii aina zote za HPV zinazosababisha saratani ya njia ya uzazi.

Habari zaidi za HPV na chanjo zinapatikana kwa njia ya mtandao wa Mpango wa Chanjo Australia (Immunise Australia Program) katika **www.immunise.health.gov.au**

Njia bora zaidi ya kuzuia saratani ya njia ya uzazi ni kupimwa mara kwa mara baada ya miaka miwili.

Kwa maelezo zaidi juu ya kupimwa njia ya uzazi, au kama unataka kubadilisha au kuondoa taarifa yako kutoka kwa orodha mkoani mwako, piga simu nambari **13 15 56** kwa bei ya simu ya kawaida.

Kama una matatizo ya kuwasiliana na kizungu, piga simu ya huduma za utafsiri nambari **13 14 50**. Hii itakugharimu sawa na kupiga simu ya karibu.

Unaweza pia kutembelea mtandao wetu kwa **www.cancerscreening.gov.au**

SWAHILI

Ulipimwa njia ya uzazi mara ya mwisho lini?

Saratani nyingi za njia ya uzazi zinaweza kuzuiliwa kama kila mwanamke angepimwa baada ya kila miaka miwili

National Cervical Screening Program
Uanzilishi wa Serikali ya Australia pamoja na mikoa

USITOE VISABABU, KUBALIANA NA DAKTARI SIKU YA KUMUONA

Je Pap Smear ni nini?

Pap Smear ni kupimwa njia yako ya uzazi kwa njia rahisi kuhakikisha ni salama. Njia ya uzazi ni mlango wa nyumba ya mototo tumboni na iko kwa ndani juu ya sehemu yako ya siri. (angalia mchoro hapo chini)

Kupimwa njia ya uzazi huchukuwa dakika chache tu na si uchungu.

Kupimwa njia ya uzazi kila baada ya miaka miwili ndio njia bora zaidi ya kuzuia saratani ya njia ya uzazi.



Kwa nini upimwe njia ya uzazi?

Kupimwa njia ya uzazi kunaweza kuonyesha dalili za saratani ya njia ya uzazi. Wakati mwingine hali ya njia ya uzazi hubadilika, na kuwa na hitilafu. Ukipimwa njia ya uzazi inaweza kujulikana kama ina hitilafu kabla haijabadilika kuwa saratani.

Nini kinachosababisha Saratani?

Kuambukizwa kwa virusi vinavyoitwa HPV (human papillomavirus) kunasababisha karibu saratani zote za njia ya uzazi. Kuna zaidi ya aina 100 tofauti za HPV. Aina mbili za HPV zinajulikana kusababisha saratani kwa karibu wote wanaougua njia za uzazi hapa Australia.

Virusi vya HPV vinapatikana kwa wingi. Watu wengi (wanne kwa watano) watakuwa na HPV wakati mmoja maishani mwao. Yeyote ambaye ashawahi kufanya ngono anaweza kuwa na HPV.

Mara nyingi, virusi vya HPV hutoweka vyenyewe baada ya miaka michache. Mara nyingine hivi virusi vinaweza vikakaa mwilini na vinaweza kusababisha saratani ya njia ya uzazi. Hii huchukuwa mda mrefu – kama miaka 10.

Kupimwa njia ya uzazi kila baada ya miaka miwili kunaweza kufanya mabadiliko ya njia ya uzazi yajulikane kabla hayajasababisha saratani. Daktari wako, muuguzi au mfanya kazi kutoka kituo cha afya anaweza kuhakikisha kuwa afya yako inafuatiliwa na unapata matibabu kama unayahitaji ili uwe na afya bora.

Nani anayehitaji kupimwa Njia ya uzazi?

Wanawake wote wa umri kati ya miaka 18 na 70 ambao wamewahi kufanya mapenzi inawabidi kupimwa njia zao za uzazi kila baada ya miaka miwili. Hata kama umewahi kufanya mapenzi na mme wako peke yake, inakubidi upimwe njia ya uzazi mara kwa mara

Je kama nimeshatolewa nyumba ya uzazi?

Ni vyema kupimwa nyumba ya uzazi kulingana na vile ulivyotolewa nyumba ya uzazi. Mshauri daktari wako, muguzi au mfanyakazi kutoka kituo cha afya kujua lipi bora nawe.

Je mtu hupimwaje njia ya uzazi?

Hivi ndivyo hufanywa

Kwanza daktari anakuuliza uvue nguo kutoka kiunoni kwenda chini na ulale chali ili akupime. Unaweza kuuliza upimwe na daktari wa kike. Halafu daktari atatumia chombo cha kupimia kufungua sehemu yako ya siri ili njia ya uzazi ionekane vyema zaidi.

Atapangusa ukuta katika njia yako ya uzazi na brashi ndogo au chombo cha kupima (kijiti kidogo ama kipande cha mpira kidogo). Kilichopanguswa kutoka njia ya uzazi, wataweka kwenye kioo kidogo na kupelekwa maabara (lebu) watakakotazama wakitumia darubini.

Je mtu husikiaje

Wakati mwingine kupimwa njia ya uzazi ni jambo la kutahayari au kuonea aibu. Kumbuka, kuwa anayekupima njia ya uzazi, hii ni kazi yake ya kawaida na hatahayari au kuona aibu.

Unapopimwa, unaweza kusikia ovyo, lakini haina uchungu. Ukisikia uchungu, mwambie daktari wako, muuguzi au mfanyakazi kwenye kituo cha afya hapohapo.

Vipi majibu?

Unapopimwa njia ya uzazi, ni muhimu umuulize daktari wako lini na vipi utapata majibu.

Majibu mengi huwa ni salama au sawa

Je kama majibu yangu sio sawa au salama

Kama majibu yako sio sawa, haimaanishi uko na saratani. Mara nyingi itakuwa una jambo dogo kama kuambukizwa ambako huisha kwenyewe bila kutibiwa.

Mara nyingine mwanamke anahitaji kupimwa njia ya uzazi mara kwa mara. Hali nyingine zisizo za kawaida zahitaji matibabu maalum. Hakikisha umeshauriana na daktari wako, muuguzi au mfanya kazi wa kituo cha afya ili akufahamishe kilicho bora kwako.